

## **MAADHIMISHO YA SIKU YA USALAMA NA AFYA MAHALI PA KAZI DUNIANI 2023 KITAIFA MKOANI MOROGORO: APRILI 26-MEI MOSI.**

Tarehe 28 Aprili ya kila mwaka hutambulika kimataifa kama siku ya Usalama na Afya mahali pa kazi ambapo Tanzania huungana na mataifa mengine duniani kuiadhimisha siku hii. Lengo kubwa la maadhimisho haya ni kuendeleza kampeni za kuhamasisha uwepo wa mazingira salama na yenye kulinda afya za watu katika sehemu za kazi. Kauli Mbiu ya Maadhimisho kwa mwakam huu ni: **Mazingira salama na afya ni kanuni na haki ya msingi mahali pa kazi.**

### **Historia fupi ya Maadhimisho haya.**

Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani chimbuko lake ni iliyokuwa siku ya Kimataifa ya kuwakumbuka waliopoteza maisha na kuumia kazini. Siku hiyo ya kuwakumbuka waathirika hao ilianza kuadhimishwa kwa mara ya kwanza mwaka 1996 huko Marekani katika Jiji la New York.

Maadhimisho hayo yalikuwa yakifanywa na Chama Cha Wafanyakazi Duniani kwa ufadhili wa Kamisheni ya Maendeleo Endelevu ya Umoja wa Mataifa. Ilipofika mwaka 2001, Shirika la Kazi Dunia liliona kuwa ni busara kubadilisha madhumuni ya siku hiyo na kuiita "Siku ya Usalama na Afya Mahali pa Kazi Duniani. Hapa kwetu Tanzania siku hii ilianza kuadhimishwa kwa mara ya kwanza mwaka 2004. Tangu wakati huo tumekuwa tukiadhimisha siku hiyo kila mwaka.

Serikali kupitia Taasisi yake ya OSHA imekuwa na desturi ya kushirikiana na wadau wa utatu (Shirikisho la Vyama Vya Wafanyakazi-TUCTA, Chama cha Waajiri Tanzania-ATE) pamoja na Shirika la Kazi Duniani-ILO katika kuratibu maadhimisho haya kitaifa.

Kwa mwaka huu, maadhimisho hayo yamepangwa kufanyika Kitaifa Mkoani Morogoro ambapo kamati shirikishi ya maandalizi kupitia vikao vyake, imekubaliana kutekeleza shughuli mbali mbali zikiwemo; Kutoa mafunzo ya Usalama na Afya kwa makundi mbali mbali ya wajasiriamali wadogo, maonesho ya Usalama na Afya mahali pa kazi, kuandaa na kutoa tuzo za kuyatambua maeneo ya kazi yanayosimia ipasavyo masuala ya usalama na afya pamoja kuwahamasisha wafanyakazi nchini kujumuika na Mgeni Rasmi siku ya kilele katika tafakari ya pamoja juu ya hali ya Usalama na Afya mahali pa kazi.

Hivyo, OSHA inapenda kuialika Taasisi yako kushiriki katika maadhimisho hayo mkoani Morogoro katika Uwanja wa Jamhuri au viwanja vingine ambavyo utaofahamishwa endapo yatatokea mabadiliko. Kushiriki maadhimisho ya mwaka huu;

- Pata taarifa kuhusu maonesho na kuwasiliana na waratibu kuweka nafasi- link (Taarifa ya maonesho) [9BfJvlz4zVxYuzN1tLclbclOPDV9HenwenZs9Ant.pdf \(osha.go.tz\)](https://www.osha.go.tz/9BfJvlz4zVxYuzN1tLclbclOPDV9HenwenZs9Ant.pdf)
- Soma tangazo la tuzo na upakue fomu ya maombi-link [6DrU55rSIRzkXk7uWCXk95iT2vSRmlgKa6sv3Z6u.pdf \(osha.go.tz\)](https://www.osha.go.tz/6DrU55rSIRzkXk7uWCXk95iT2vSRmlgKa6sv3Z6u.pdf)
- Jisajili kushiriki maonesho/tuzo kwa njia ya mtandao (WIMS)- link; soma mwongozo wa kutumia mfumo  
Bofya kutazama muongozo wa kujisajili  
[9TCifBPlv53OYbXgAg64nUE7UGq3soe2AjVHAhQg.pdf \(osha.go.tz\)](https://www.osha.go.tz/9TCifBPlv53OYbXgAg64nUE7UGq3soe2AjVHAhQg.pdf)  
Bofya kujisajili [OSHA | Wims](https://www.osha.go.tz/wims)

## **WORLD DAY FOR SAFETY AND HEALTH AT WORK COMMEMORATIONS 2023 WILL BE HELD AT NATIONAL LEVEL IN MOROGORO: APRIL- MAY 01<sup>st</sup>.**

Tanzania will join other countries across the world to commemorate the World Day for Safety and Health at Work on the 28<sup>th</sup> April, 2023. This year's theme is; **A safe and health working environment is a fundamental principle and right at work.**

### **Safety Day History**

The World Day for Safety and Health at work originated from the International Commemoration Day for Dead and Injured Workers, organized worldwide by the Trade Union Movement since 1996. It was celebrated for the first time at Newyork City in the United States of America under the sponsorship of the United Nations Commission on Sustainable Development (CSD).

When it reached 2001, the International Labour Organisation (ILO) saw it necessary to change the purpose of the day and hence named it 'World Day for Safety and Health at work'. In Tanzania, we started celebrating the day in 2004. Since then, we have been celebrating the day in every year.

In this year, the commemorations will be held at national level in Morogoro Region. In marking the day, **OSHA** in collaboration with the **Association of Tanzania Employers (ATE)**, **Trade Union Congress of Tanzania (TUCTA)** and the **International Labour Organisation (ILO)** has arranged to executed a couple of activities as part of safety and health promotion campaign.

The activities include; Occupational Safety and Health exhibitions for employers and workers to showcase OSH Management systems, Awards for Occupational Safety and Health (AOSH) competition among workplace occupiers/employers who are effectively implementing the OSH Act, 2003, Occupational Safety and Health training to some industrial workers, small-scale miners, small-scale entrepreneurs as well as persons with disability.

Also, the celebrations will involve mobilizing workers to be available during the climax of the commemorations on 28<sup>th</sup> April, 2023 at Jamhuri Stadium in Morogoro. The event will be officiated by the **Minister of State in the Prime Minister's Office (Labour, Youth, Employment and Persons with Disability)**, Hon. Prof. Joyce Ndalichako.

To participate in this year's Safety Day activities;

- Find OSH exhibition details and call event coordinators to book pavilion space- link [9BfJvlz4zVxYuzN1tLclOPDV9HenwenZs9Ant.pdf \(osha.go.tz\)](#)
- Read an advert on the Awards for Occupational Safety and Health (AOSH-2023) and download an application form- link [6DrU55rSIRzkXk7uWCXk95iT2vSRmlgKa6sv3Z6u.pdf \(osha.go.tz\)](#)
- Register online to participate in exhibitions and AOSH-2023 through WIMS- link Click below to see user guide [9TCifBP1v53OYbXgAg64nUE7UGq3soe2AjVHAhQg.pdf \(osha.go.tz\)](#)  
Click to register [OSHA | Wims](#)